PrecisionAir
YOU ARE WHY WE FLY

# TAARIFA YA MWENYEKITI

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TATU WA WANAHISA**
**FEBRUARI 18, 2015**

Mabibi na Mabwana,

Nachukua nafasi hii kuwakaribisha nyote kwenye mkutano wetu mkuu watatu wa wanahisa. Kwaniaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Precision Air, najisikia fahari kubwa kuwasilisha kwenu ripoti ya kampuni ya mwaka kwa mwaka ulioishia tarehe 31Machi 2014.

Tutaanza mkutano wa leo kwa kupitia ripoti ya fedha kwa mwaka 2014 , kabla ya kuendelea na taratibu rasmi za mkutano.

Mwisho wa mkutano nitawakaribisha kujumuika pamoja nasi kupata kifungua kinywa pamoja na majadiliano baina yetu na kufahamiana zaidi.

Kabla hatujaanza ningependa kuitambulisha kwenu Bodi ya Wakurugenzi. Kwa kuanzia kulia ni;

- Ndugu Titus Naikuni - Mjumbe
- Ndugu Vincent Shirima - Mjumbe
- Bibi Elizabeth Minde - Mjumbe
- Ndugu Manzi Rwegasira - Mjumbe
- Ndugu Ron Schipper - Mjumbe
- Bibi Sauda Rajab - Mjumbe
- Imani Kaduma - Katibu

Kwenye mkutano mkuu wa mwaka jana niliwaeleza juu ya safari ambayo PW tumesafiri hadi tulipo hapa sasa, nakuainisha mafanikio pamoja na changamoto tulizokumbana nazo njiani.

Moja ya mafanikio amabayo yalijionyesha dhahiri ni pamoja na kukua kwa amana mfululizo kwa kipindi cha miaka kumi, matokea ya soko la hisa kwa mwaka 2011, msukosuko wa uchumi wa dunia na athari za bei za mafuta kwenye sekta ya anga.

Nilisisitiza kwa mapana na marefu juu ya mpango mabadiliko na mpango mkakati wa miaka 5 ambao uliundwa kukabiliana na matatizo makuu manne

kama yalivyo ainishwa hapo awali, ambayo ni ; mtandao wa safari sizisizo na tija, Ndege zililizo na gharama kubwa za uendeshaji, uzalishaji hafifu pamoja na fursa za mapato zisizo tumika sawia, Pamoja na mpango wa mda mrefu wa kutafuta mataji kwaajili ya kuendeleza biashara. Mikakati hii iliunda misingi ya utendaji ndani ya Precision Air.

Mazingira ya biashara yameendelea kuwa ya ushindani mkubwa na yenye changamoto, huku kukiwa na hofu juu ya usalama duniani kote na kuathiri biashara ya usafirishaji duniani kwa ujumla. Pia thamani ya fedha za kigeni hususani Dola ya Kimarekani imeendelea kukua ikilinganishwa na fedha yetu ya ndani nakupelekea akiba hafifu ya fedha za kigeni na hasara kwa biashara ambazo matumizi yake mengi yanategemea fedha za kigeni.

Pamoja na changamoto zote hizi, PW imeweza kusimamia thabiti mipango mkakati yake na matokeo yake kwa mwaka wa fedha  ulioishia tarehe 31 Machi 2014 kampuni ilipata hasara ya Shilingi za Kitanzania bilioni 12 ikiwa nimafanikio kwa asilimia 60% ikilinganishwa na hasara ya Shilingi bilioni 30 iliyopatikana mwaka uliotangulia .

Kufuatia upitiwaji wa mtandao wetu wa safari kama ilivyo ainishwa hapo juu, baadhi ya safari zilizokua hazina au kutoa mchango mdogo katika pato la kampuni, zilifanyiwa mabadiliko au kuondolewa kabisa kwenye matandao wetu. Hili lilipelekea moja kwa moja kupungua kwa idadi ya abiria walio safiri na ndege zetu pamoja na pato kutokana na safari hizo.

Hata hivyo kampuni iliweza kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji, ambapo punguzo hilo lilipelekea kuongezeka kwa faida kabla ya kodi kwa asilimia 28 kwa mwaka 2014, ikilinganishwa na asilimia 18 iliyopatikana mwaka 2013, hii ikiwa ni pamoja na kufanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa cha hasara.

Ushindani kwenye soko la ndani uliendelea kuwa sababu ya kupanga viwango vya nauli kwa abiria, lakini kinyume na imani ya wengi  kwamba nauli zingeshuka, kumekua na ongezeko la viwango vya nauli kwa asilimia 7.

Upatikanaji wa mtaji  wa muda mrefu kuendeleza biashara, umeendela kua na changamoto kwa mwaka 2014. Juhudi zinaendelea kuhakikisha upatikanaji wa suluhisho wa tatizo hili kwani hakukuwa na mtaji wowote uliopatikana kwa kipindi chote hiki. Hali hii imepelekea kusuasua kwa utekelezwaji wa baadhi ya mikakati, hususani ukarabatwaji kwa wakati wa ndege ili kuongeza matumizi ya ndege kwa asilimia 100.

Kampuni kwa muda wote huu ilitumia asilimia 70 tu ya ndege zake ilizo nazo na hivyo kupoteza fursa ya kutenegeneza pato zaidi na kuzuia hasara zaidi.

Matarajio ya badaye:

Kampuni itaendelea kusimamia thabiti utekelezwaji wa mpango mkakati wake wa miaka mitano kama ulivyopitishwa na Bodi, hii ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa kila mwezi wa utekelezwaji wa mikakati hiyo kama ilivyo ainishwa.

Kwa kuzingatia hilo, Kampuni itaendelea kujikita katika kuboresha upatikanaji wa faida na fedha za uendeshaji wa biashara kwa kuongeza pato na kupunguza gharama za uendeshaji katika kiwango kinachokubalika.

Kampuni itajikita katika yafuatayo;

- Kupitia mtandao wetu wasafari na kuangalia uwezekano wa kufungua fursa mpya za kuongeza idadi ya abiria wanaosafiri na ndege zetu hivyo kuongeza pato la ziada kupitia ndege tulizonazo.
- Kupitia upya ujuzi wa wafanyakazi wetu na kuuboresha kupitia mafunzo au kuajiri watu sahihi katika vitengo sahihi.
- Kampuni itaendelea kusimamia kwa makini gharama za uendeshaji katika vitengo vyote.
- Kuongeza ushirikiano na makampuni mengine ya ndege kupitia mikataba maalumu ili kuongeza idadi ya abiria pamaoja na pato.
- Kukamilisha makubaliano ya ushirikiano katika kutoa huduma kwenye viwanja vya ndege kwa mashirika mengine, ili kuzalisha mapato ya ziada kama ilivyo ainishwa.

Kwa utekelezwaji wa maazimio tajwa hapo juu kampuni inatarajia matokeo yafuatayo;

- Kuongezeka kwa idadi ya abiria watakao safari nasi na hivyo kupelekea ongezeko katika pato.
- Kuongezaka kwa ujuzi na uwezo wa wafanyakazi wetu na nimatumaini yetu kuwa kutapelekea kuongezeka kwa uzalishaji.
- Kufanikiwa katika usimamizi wa gharama na uboreshwaji wa huduma zetu ili kuongeza pato kwa kampuni pamoja na kutoa huduma iatakayo mridhisha mteja.

Kwa kuongezea kwa niliyotaja hapo juu, kampuni imeweka mkakati na kampuni ya matengenezo kuhakikisha inafanyia ukarabati injini zote zinazo hitaji matengenezo na kwamba ifikapo mwezi julai ndege zote ziwe zinafanya kazi. Mpango huu utatupa uwezo wakutoa huduma iliyoboreka na ya uhakika nakurudisha mwenekano wa kampuni kama kampuni ya mfano wa kuigwa katika huduma za anga.

Ili kupunguza mzigo wa madeni ya ndege amabyo yanaikabili kampuni kwa sasa, kampuni iko katika mazungumzo na mwekezaji ilikukamilsha makubaliano ya kununua ndege zenye madeni na kisha kuzikodisha kwa kampuni (Sale and lease back) Makubaliano haya yanatarajiwa kufikiwa mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka huu.

Pia kampuni haijakata tama kutafuta mtaji mkubwa wa muda mrefu, jitihada madhubuti zinaendelea kuhakikisha upatikanaji wa mtaji huo kupitia wanahisa wa sasa au wawekezaji wasio wanahisa.

Michael Shirima
Chairman
Bodi ya Wakurugenzi Precision Air
**18 February 2015**

---